# THE CURVE EVALUATION TEST

## K.C.P.E TRIAL -2020

SILVER 002

# -KISWAHILI-
# SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### Muda: Saa 1 Dakika 40

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu
9. Kwa kila swali 1-50 uniepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

19. Kamilishi methali: Ukiona vyaelea jua__________

    A. vyaenda

    B. vimeundwa

    C. vyazima

    D. vyaisha

**Jibu sahihi ni B.**

**19.** [A] [~~B~~] [C] [D] **20.** [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

© *umetungwa na kuchapishwa na Tangent Ventures*

**FUNGUA UKURASA**

*Kwa kila nafasi 1 - 15, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Tulikaa mkabala na kidimbwi _____1_____ upepo na kutazama runinga. Kipindi tulichokitazama kilifanya nyoyo kuatuka _____2_____ jitimai. Tuliona watoto wadogo ambao hali zao _____3_____. Vifupa vya mbavu _____4_____ viliweza kuhesabiwa na matumbo yao yalikuwa _____5_____ viriba. "Kwa nini watoto hawa huwa hivi?" Baraza _____6_____. Maganga akajibu, "Hawa wanaugua ugonjwa wa utapiamlo. Utapiamlo ni _____7_____ wa lishe bora mwilini. Tukila chakula _____8_____ mahitaji ya mwili, tutashikwa na ugonjwa huu."

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. tukifunga | B. tukipunguza | C. tukipunga | D. tukifungia |
| 2. | A. na | B. kwa | C. katika | D. kwenye |
| 3. | A. zilihuzunisha | B. zilihuzunika | C. zilihuzishana | D. zilinihusunisha |
| 4. | A. vyao | B. zao | C. lao | D. yao |
| 5. | A. mithili za | B. mithili wa | C. mithili na | D. Mithili ya |
| 6. | A. alishauri | B. alijisaili | C. alisaili | D. alijiuliza |
| 7. | A. upungufu | B. upunguzaji | C. kupunguza | D. kupungua |
| 8. | A. kisichotoshana | B. kisichotosheka | C. kisicholahewa | D. kisichotosheleza |

Baada ya mtoto kuzaliwa, Mungu _____9_____ walimu wengi. Mwalimu wa kwanza wa mtoto ni mama. Yeye _____10_____ anayeanza kuujaza ukurasa _____11_____ wa ubongo wa mwanawe. Baba pia ana _____12_____ kubwa katika kumfunza na kulea mtoto. Mazingira ya mtoto _____13_____ yeye huanza kuwa na walimu wengi wa _____14_____. Ikumbukwe kuwa _____15_____ mazingira anapokulia mtoto yatamfunza maadili mema yeye ataibuka kuwa mwadilifu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. hutunukiwa | B. humtunukia | C. huwatunukia | D. anatunukiwa |
| 10. | A. ndio | B. ndiwe | C. ndiyo | D. ndiye |
| 11. | A. tupu | B. mtuvu | C. mtupu | D. tulivu |
| 12. | A. madaraka | B. dhima | C. wajibu | D. wadhifu |
| 13. | A. yanapopanuka | B. inapopanuka | C. zinapopanuka | D. anapopanuka |
| 14. | A. kuigiwa | B. kuigana | C. kuigizana | D. kuiga |
| 15. | A. hata kama | B. ijapokuwa | C. iwapo | D. ingawa |

**23.** Kanusha kwa kutumia ***'-to-'***

***Kusoma kwake kulimfaa mtihanini***

A. Kutosoma kwake hakukumfaa mtihanini

B. Kutosoma kwake kulimfaa mtihanini

C. Kusoma kwake hakutomfaa mtihanini

D. Kutosoma kwake hakutomfaa mtihanini

**24.** Chagua msemo unaofafanuliwa na maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo:-

Majirani wale **hawaelewani kabisa**

A. Ni wa kufa kuzikana

B. Hawana mbele wala nyuma

C. Hawapikiki katika chungu kimoja

D. Wanapaliana moto.

**25.** Tumia vitate vifaavyo zaidi kukamilisha sentensi hii. Mzee Mwamburi alii ___ile ___yake majini na kuisafisha; hatimaye akahudhuria ___isiyokuwa na___

A. toza, tosa, ndoa, doa

B. tosa, toza, ndoa, doa

C. tosa, toza, doa, ndoa

D. toza, tosa, doa, ndoa

**26.** Andika wingi wa sentensi hii

***Ubele wa kuku umeng'oka***

A. Mabele ya kuku yameng'oka

B. Bele za kuku zimeng'oka

C. Mabele za vikuku zimeng'oka

D. Bele ya kuku imeng'oka

**27.** Ni sentensi ipi si sahihi kati ya hizi?

A. Nunua gari maadamu una pesa

B. Siendi sokoni wala mtoni

C. Mvua hunyesha aghalabu nyakati za jioni

D. Shamba letu linaanzia hapa wala pale

**28.** Mfupa wa bega wa mbele katika mwili wa binadamu huitwa______

A. muundi

B. fuvu

C. mtulinga

D. nguyu

**29.** Kinyume cha neno ***kutabasamu*** ni ________

A. kucheka

B. kulia

C. kukasirika

D. kununa

**30.** ***'Ukimwona Rehema, mpashe salamu zangu,'*** Hii ina maana kuwa

A. hatampasha salamu zozote hata akimwona.

B. asipomwona Rehema hatampasha salamu.

C. kumwona kwake Rehema kutampasha salamu.

D. asipompasha salamu hatamwona Rehema.

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo***

**16.** Kutokana na kitenzi **soma**, tunapata mnyambuliko **somesha**. Je, kutokana na kitenzi **kimbia** tunapata________

A. kimbisha

B. kimbilia

C. kimbiziwa

D. kimbiza

**17.** Darasa letu lina wanafunzi 32. Thumni ya wanafunzi hawa hawafahamu Hisabati vyema, nao subui ya waliosalia wanatatizika katika ngeli za Kiswahili. Wengine wote wanajimudu vyema katika masomo yote. Je, ni wanafunzi wangapi wasio na matatizo kimasomo?

A. 4 B. 8

C. 28 D. 24

**18.** Unapomtembelea mgonjwa hospitalini utamwambiaje?

A. Samahani

B. Ugua pole

C. Makiwa

D. Ugua polepole

**19.** Mshonaji nguo anapotaka kumpima mteja nguo atatumia kifa gani?

A. Dira

B. Rula

C. Utepe

D. Mizani

**20.** Tumia nomino za makundi kwa usahihi ili kukamilisha sentensi hii. *Nilipotoka nje kuchukua ____cha funguo kutoka garini, niliona ___la moshi kutoka mbali*

A. kichala, wingu

B. kicha. shungi

C. kicha, wingu

D. kipeto, fundi

**21.** Ni sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo ambayo huonyesha matumizi ya 'ritifaa?

A. Kuonyesha kuwa kuna orodha itakayofuata


B. Kuungia sentensi mbili zinazoweza kujitegemea au kusimama peke yake.

C. Kuonyesha kuwa neno lililokatishwa linaendelea katika mstari unaofuata.

D. Kuonyesha kuwa neno limefupishwa ama kuonyesha sauti ya ving'ong'o

**22.** Taja majina ya maumbo haya

i ii



| i | ii |
|---|---|
| A. kuru | geli |
| B. pia | hilali |
| C. duara | kuru |
| D. kuru | mviringo |

*Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40 yanayofuata.*

Johana Namusonge.

S.L.P. 18,

SALAMA.

26 Februari 1996.

Kwa mwanangu Tina.

Pokea salamu nyingi kutoka kwangu. Baada ya salamu hizo ningependa kukuarifu ya kwamba nimepata barua yako ya tarehe 16 Februari 1996.

Nafurahi kusikia kuwa mmeanza masomo yenu ya kidato cha kwanza. Natumaini utaendelea kusoma kwa bidii kama mwaka jana ulipokuwa katika darasa la nane. Kumbuka kuwa inakubidi sana katika masomo yako, kutii sheria zote za shule na kutangamana vyema na wanafunzi wenzako. Bila shaka wayafahamu hayo, maana wewe si mtoto mdogo tena kwani unaweza kupambanua jema na baya. Lakini inafaa wanadamu kukumbushana.

Katika barua yako umenung'unika kuwa chakula hicho hakiivi sawasawa. Hapo sikubaliani nawe kwa sababu haiwezekani kuwa kila siku mnakula chakula aina moja. Nafikiri unatia chumvi. Kule kutoiva kwa chakula mara kwa mara si jambo lisilokuwa la kawaida. Hata huku nyumbani mara nyingine chakula kikipikwa huwa hakiivi kabisa ama hukosa chumvi au viungo.

Aidha, ni muhimu kushiriki katika shughuli zote za shuleni kama vile michezo, mashindano ya aina mbalimbali na pia ibada. Usisahau kwamba elimu sio kusoma na kuhitimu peke yake, bali ni mchanganyiko wa mambo yote mazuri utakayojifunza shuleni mwako.

Sina mengi zaidi ya hayo. Hivi karibuni utapokea hati ya pesa kwa posta ambazo zitakusaidia kwa masurufu yako.

Pokea salamu kutoka kwa mama yako na ndugu zako. Usikose kutuandikia barua mara kwa mara kutujulisha hali yako.

Mpenzi baba yako

John Namusonge

31. Baba alimwandikia mwanawe barua muhula upi?
A. Wa kwanza
B. Wa pili
C. Wa tatu
D. Haijulikani

32. Mtoto anayeandikiwa barua na babake
A. alikuwa anachezea masomo katika darasa lake
B. hakujitahidi sana katika darasa la nane
C. alikuwa amefanya vibaya katika mtihani wake wa darasa la nane
D. alikuwa amefanya vizuri katika mtihani wake wa darasa la nane

33. Tina ananung'unika kuwa chakula cha shule
A. wakati mwingine hakiivi vizuri
B. hakiivi kabisa siku zote
C. hakina viungo
D. hakiliki

34. Neno ***bidii*** kama lilivyotumika katika barua hii lina maana sawa na ***juhudi***. Neno jingine lipi lenye maana sawa na ***sheria***
A. Mwenendo
B. Kawaida
C. Kanuni
D. Maelezo

35. Babake Tina
A. anakubaliana na mwanawe katika kunung'unika kwake
B. anamkanya mwanawe asiwe na tabia ya kunung'unika.
C. anasisitiza kuwa mwanawe hana adabu na bidii
D. anasisitiza kuwa mwanawe hatii sheria za shule

36. Ni maelezo yapi ambayo si sahihi?
A. Baba anatilia mkazo kuwa kusoma ni muhimu.
B. Baba anamwambia mwanawe awe na adabu daima.
C. Baba anamkumbusha mwanawe kuwa ni muhimu kuwa na bidii katika masomo
D. Baba anamshauri mwanawe awajali wanafunzi wenzake tu.

37. Katika barua hii tunaona kuwa chakula kinachopikwa nyumbani
A. hakipikwi barabara
B. kawaida hakiongezwi chumvi
C. hakitofautiani sana na kile cha shule
D. hakiongezwi chumvi na hakina ladha.

38. Baba huyu ana tabia gani?
A. Anayependa mtoto wake na elimu kwa jumla
B. Mkali na anayependa kazi
C. Mtedekezaji asiyependa mtoto kusoma tu
D. Asiyependa manung'uniko na shule za bweni

39. Kwa nini baba anasisitiza mwanawe ashiriki katika shughuli za shuleni?
A. Anataka mwanawe awe mwana michezo mashuhuri
B. Anaonelea kuwa elimu sio kusoma vitabu peke yake
C. Anafikiri ni vyema kushindana shuleni
D. Anaamini elimu ni kuvumilia shuleni

40. Ni methali gani kati ya hizi inayofafanua vizuri ujumbe wa barua hii?
A. Mcheza kwao hutuzwa
B. Aliye juu mngoje chini
C. Akili nyingi huondoa maarifa
D. Mtaka cha mvunguni sharti ainame

*Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.*

Ama kwa hakika katika **mwongo** huu wa kufunga karne ya ishirini tumeshuhudia dunia yetu ikicharazwa kwa mikasa mithili ya mtoto aliyepotoka adhibiwavyo na mzazi. Kadri upotovu wa mtoto uendeleavyo kuongezeka ndivyo sababu nayo inavyoongezeka mpaka mabadiliko mema yapatikane.

Si jambo la mjadala tena kusema kuwa kwa jumla walimwengu wa sasa ni wapotovu kuliko wale wa miaka hamsini iliyopita. Licha ya hivyo misikiti na makanisa hujaa waumini tele. Hawa husomewa maandishi matakatifu na kusisitizwa umuhimu wa maadili kila mara. Inaonekana ni kweli sikio la kufa halisikii dawa. Wengi wameyatia masikio yao pamba,hawasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

Je, kuna uhusiano kati ya kudidimia kwa uadilifu na mikasa iliyokumba dunia yetu katika mwongo huu? Watu wengi wanaamini upo uhusiano.

Nchi ya Marekani katika jimbo la Kalifonia barabara moja kuu ilipasuliwa na mtetemko mkubwa wa ardhi. Watu waliokuwa katika safari zao wakaangamia. Baadaye mji wa Kobe kule Ujapani uliharibiwa sana na mtetemko mwingine. Mwaka jana sehemu ya Kaskazini mwa Uturuki ilikumbwa na balaa hili na maelfu waliachwa bila makao. Baadaye, nchini jirani ya Ugiriki ilipata maafa kama hayo. Katika nchi yetu kumekuwa na ongezeko la maradhi,mafuriko na kiangazi cha kutisha.

Ni nani asiyekumbuka gharika iliyoenea Marekani ya kati mwaka huo huo? Mito ilifurika kutokana na mvua kubwa, maji yakaleta maafa makubwa nchini Guatemala, Nikaragua na kwingineko.

Nchi za Ulaya nazo zilipatwa na janga tofauti. Katika majira ya kiangazi baadhi ya nchi zilizidiwa na joto. Katika Uhispania na Ufaransa iliwabidi watu wengi wahame makazi yao wakimbilie sehemu zenye milima angalau wapate nafuu ya baridi.

Bara la Afrika nalo halikubahatika. Mvua kubwa ambayo haijawahi kunyesha kwa miongo ya miaka imewaua mamia ya watu Afrika Kusini na Msumbiji katika mwaka wa elfu mbili. Wakati mwingi mikasa hii haiwezi kuzuilika kwa sababu Mola tu ndiye aliye na uwezo huo. Lakini uharibifu wa hali ya anga na ukataji ovyo wa miti umechangia haya yote.

41. Maneno yenye maana ya **mwongo** ni

A. Miaka hamsini

B. Miaka kumi

C. Miaka elfu moja

D. Miaka tano

42. Mabadiliko mema ya mtoto mpotovu

A. huzidisha adhabu

B. huendeleza upotovu

C. huendeleza adhabu

D. hupunguza adhabu

43. ***"Si jambo la mjadala tena"*** ina maana kuwa

A. si swala la kubishaniwa

B. si swala lenye maana

C. si swala la kutangaziwa

D. si swala lenye masharti.

44. Uovu umeendelea duniani hata baada ya

A. makanisa na misikiti kuongezeka

B. wakristo na waislamu kuelewana

C. waumini wa dini kuongezeka

D. waumini wa uongo kupungua

45. Maana ya methali ***sikio la kufa halisikii dawa*** ni

A. asiyesikia hasikii

B. asiyetii ni vigumu kumkanya

C. sikio la kufa halitibiwi

D. asiyesikia haambiwi

46. Mwandishi anaamini kuwa

A. hakuna uhusiano kati ya uovu na maafa

B. hakuna uhusiano kati ya dini na maafa

C. kuna uhusiano kati ya uovu na maafa

D. kuna uhusiano kati ya dini na maafa.

47. Mitetemeko ya ardhi iliharibu

A. Sehemu ya Uturuki, Kalifonia na Ugiriki

B. Sehemu za Ujapani, Guatemala na Nikaragua

C. Sehemu za Kalifonia, Ujapani na Uturuki

D. Sehemu za Kalifonia, Ugiriki na Guatemala

48. Mafuriko yaliyoenea Marekani ya kati yalitokana na

A. mawimbi ya baharini

B. mvua ya rasharasha

C. mawimbi ya upepo

D. mvua ya gharika

49. Iliwabidi wazungu wakimbie makwao ili wajinusuru kutokana na

A. baridi kali

B. mvua kubwa

C. joto jingi

D. mitetemeko ya ardhi

50. Nchi mbili za Afrika zilizoathiriwa na mafuriko ni

A. Uturuki na Ugiriki

B. Msumbiji na Afrika Kusini

C. Ujapani na Msumbiji

D. Guatemala na Ujapani